



**HATUA ZA KUZINGATIA KWA WAINGIZAJI TAIRI ZILIZOTUMIKA NA MPYA ZA
VYOMBO VYA MOTO ILI KUPATA KIWANGO KILICHOTHIBITISHWA
NA TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR**

UTANGULIZI.

Taasisi ya viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa Sheria namba 1 Sheria ya Viwango vya Zanzibar ya mwaka 2011 ikiwa na jukumu la msingi la kuandaa viwango vya bidhaa na huduma ili kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinakidhi ubora wa viwango husika.

ZBS imeanzisha mfumo wa ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi (Pre-Verification of Conformity - PVoC) kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi zikiwemo michele, sabuni, mafuta nk. Ama kwa bidhaa ambazo zinaongizwa ndani ya nchi bila ya kukaguliwa zilipotoka hukaguliwa kwa mfumo wa ukaguzi wa ndani (Destination Inspection - DI) kwa bidhaa kama vile magari yaliyotumika, matairi na nyenginezo.

Kutokana na uingizwaji wa kiwango kikubwa cha matairi yaliyotumika yaliyo chini ya kiwango ZBS imeandaa mfumo wa ukaguzi na usaili kwa waingizaji wa tairi zilizotumika na kutaarisha muongozo maalum ili wapate uelewa juu ya tairi hizo. Muongozo huo unaeleza juu ya mambo muhimu na ya msingi ambayo mnunuaji yampasa kuzingatia, kama ifuatavyo:-

1. Mwaka uliotengenezwa;
2. Hali ya tairi (mfano, ulikaji wa kashata, mipasuko, kufanya uvimbe n.k.)
3. Ukubwa wa kashata (haitakiwi kashata iwe chini ya milimita 1.6)

4. Aina ya tairi (tari zinazotakiwa kuingizwa nchini ni zinazokubalika kwa matumizi ya miongo yote ya hali ya hewa yaani sehemu zenye hali ya ubaridi na ujoto)

Wito kwa waingizaji wa matairi

ZBS inawaomba waingizaji kufuata na kuutumia vyema muongozo wa kuingiza tairi zilizotumika ili kufanikisha uingizaji wa bidhaa hizo wenye lengo la upatikanaji wa bidhaa salama na zenye Ubora na viwango katika soko la Zanzibar.

Lengo la kuwa na muongozo huu ni:-

- Kumlinda mtumiaji wakati wa matumizi
- kuhakikisha bidhaa za tairi zilizotumika zinazoingizwa nchini ni zenye ubora na za kiwango yenye ubora ili kuilinda jamii na madhara ya tairi zilizo chini ya kiwango.
- Kupunguza wimbi la uingizwaji wa tairi zilizochini ya kiwango
- Kuyatunza mazingira ya nchi yetu
- Kuongeza kipato kwa watumiaji kwa kutumia bidhaa zilizo na kiwango.









